110

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

Anuani ya simu "ELIMU"
Simu: 026 296 35 33
Baruapepe:info@moe.go.tz
Tovuti: www.moe.go.tz

Mji wa Serikali,
Eneo la Mtumba,
Mtaa wa Afya,
S. L. P. 10,
**40479 DODOMA.**

Unapojibu tafadhali taja:

**Kumb.Na. ED/OKE/NE/W/Vol/1/72**

**Tarehe: 08 Januari, 2021**

Katibu Mkuu,
Ofisi ya Rais -TAMISEMI,
Mji wa Serikali Mtumba,
Mtaa wa TAMISEMI,
S.L.P 1923,
**41185 DODOMA.**

**Yah: UTEKELEZAJI WA WARAKA WA ELIMU NA, 1 WA MWAKA 2021 KUHUSU KUFUNDISHWA KWA SOMO LA HISTORIA YA TANZANIA KAMA SOMO LA LAZIMA KWA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI NCHINI**

Mada tajwa hapo juu yahusika.

2. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WyEST) imeandaa Waraka tajwa wa kuanzishwa kwa somo la **Historia ya Tanzania** ili lifundishwe kama somo la lazima kwa Shule za Msingi na Sekondari hapa nchini. Somo hilo linatakiwa kufundishwa kuanzia ngazi ya Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari.

3. Lengo la kufundishwa kwa somo la Histoia katika shule zetu ni kuwajengea wanafunzi moyo wa uzalendo kwa ustawi wa Taifa letu.

4. Kwa barua, hii unaombwa kuwatumia wadau wote wa elimu wa shule za umma Waraka ulioambatishwa ili kuanza kutekeleza agizo la Waraka huo. Wizara ina imaini kuwa Waraka huu utakuwa ni nyenzo ya kuwaandaa vijana wetu kuwa raia wema wa nchi yao.

5. Asante kwa ushirikiano.

Jonathan M. Kabengwe

**KAIMU KATIBU MKUU**

**WARAKA WA ELIMU NA. 1 WA MWAKA 2021**
**UTARATIBU WA KUANZISHA NA KUENDESHA KLABU ZA SOMO LA HISTORIA KATIKA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI**

Mafanikio ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni katika nchi yoyote ile duniani yanachangiwa na sababu mbalimbali. Moja ya sababu kubwa za mafanikio hayo ni namna nchi husika ilivyofanikiwa katika kujenga moyo wa uzalendo kwa wananchi wake. Kwa kuzingatia hilo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli mnamo tarehe 9.12.2020 wakati akiwaapisha Mawaziri na Naibu Mawaziri IKULU – CHAMWINO, DODOMA alitoa agizo la kufundishwa kwa somo la Historia ya Tanzania kama somo la lazima kwa wanafunzi wote.

Katika kutekeleza agizo hilo, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeandaa Waraka wa Elimu Na.1 wa Mwaka 2021 unaoelekeza namna ya kujenga moyo wa uzalendo kwa wanafunzi kupitia somo la Historia ya Tanzania. Kutakuwa na mikakati ya aina mbili katika kutekeleza agizo hilo: (1) Mkakati ya Muda Mfupi (2) Mkakati ya Muda Mrefu. Waraka huu unajikita katika utekelezaji wa Mkakati ya Muda Mfupi unaohusu **Uanzishwaji wa Klabu za Somo la Historia ya Tanzania na Uzalendo**. Mkakati wa Muda Mrefu unahusu mapitio ya Mitaala ya Somo la Historia ya Tanzania. Mapitio hayo yatakapokamilika Wizara itatoa maelekezo kuhusu utekelezaji wa Mitaala hiyo.

**Mambo ya Kuzingatia katika Uanzishaji na Uendeshwaji wa Klabu za Somo la Historia Shuleni**

Klabu za Somo la Historia ya Tanzania na Uzalendo zitaanzishwa katika ngazi za Elimu ya Awali, Shule za Msingi na Sekondari. Katika kuendesha Klabu hizo:

(i) Mahudhurio kwa kila mwanafunzi ni ya lazima;
(ii) Klabu zitaendeshwa katika muda wa ziada;
(iii) Klabu zitafanya mambo mbalimbali kuendana na ngazi ya elimu kama vile majadiliano, nyimbo, hadithi/simulizi, mashairi, ngonjera na kutembelea maeneo ya historia;
(iv) Kusoma vitabu vya Historia ya Tanzania;
(v) Kusikiliza vipindi vya Radio na Televisheni vitakavyoendeshwa na TET (Mfano Hotuba za viongozi mbalimbali na kuzitafakari zikiwemo zile za viongozi wastaafu wa awamu ya kwanza hadi ya nne na hotuba za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli;
(vi) Kualika wageni mashuhuri kama vile wazee wanaofahamu Historia ya Tanzania na viongozi shuleni; na

(vii) Matumizi ya Kaulimbiu mbalimbali kila mwalimu anapoingia darasani na wakati wa Klabu za Somo la Historia ya Tanzania na Uzalendo. Baadhi ya Kaulimbiu hizo zimeambatishwa na Waraka huu (Kiambatisho Na. 1).

Walimu na wanafunzi wanahimizwa kuwa wabunifu katika kutunga Kaulimbiu nyingine zenye malengo sawa na haya.

Waraka huu unaanza kutumika kuanzia tarehe 11 Januari, 2021.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
**KAMISHNA WA ELIMU**

KIAMBATISHO NA. 1

## KAULI MBIU

1. Uhuru ni tunu yetu tuudumishe na kuulinda.
2. Tulinde rasilimali zetu, tuwe wazalendo na tukemee rushwa na uzembe.
3. Naipenda nchi yangu, nitaitumikia na nitaiendeleza kwa moyo wangu wote.
4. Tanzania nakupenda sitashawishika kukuhujumu.
5. Mimi ni mtanzania, nitadumisha utaifa wa taifa langu na uzalendo wa nchi yangu.
6. Nitailinda na kudumisha tamaduni zinazolinda utu na maadili ya Mtanzania.
7. Tanzania kwanza, uchumi wa viwanda kwa maendeleo ya Taifa.
8. Maendeleo ya nchi yangu yanaanza na mimi mwenyewe.
9. Mimi ni mlinzi wa rasilimali za nchi yangu.
10. Binadamu wote ni ndugu zangu na Afrika ni moja.
11. Nitaitumikia nchi yangu na watu wake kwa moyo wangu wote.
12. Nitajitolea nafsi yangu kuondoa umaskini, ujinga, magonjwa na dhuluma.
13. Rushwa ni adui wa haki, Sitapokea wala kutoa Rushwa.
14. Nitajielimisha kwa kadri ya uwezo wangu na kutumia elimu yangu kwa ajili ya maendeleo ya nchi yangu.
15. Nitashirikiana na Watanzania wenzangu kuijenga na kuitetea nchi yangu.
16. Nitakuwa raia mwema na mwaminifu kwa nchi yangu daima.